



**CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO TANESCO  
(TANESCO SACCOS LTD)**

**NAMBA YA KUANDIKISHWA: 1843**

**SERA YA MIKOPO**

TANESCO SACCOS LTD  
S.L.P 54231  
DAR ES SALAAM  
Simu: 0222401033  
Email: [info.saccos@tanESCO.co.tz](mailto:info.saccos@tanESCO.co.tz)

2019

## YALIYOMO

UTANGULIZI.....	1
SEHEMU YA KWANZA .....	3
1. SERA YA MIKOPO.....	3
1.1. Utangulizi .....	3
1.2. Madhumuni ya Sera ya Mikopo.....	3
1.3. Walengwa wa Sera hii .....	3
1.4. Misingi ya Utoaji wa Mikopo kwa Wanachama.....	4
1.5. Taratibu za Utoaji Mikopo .....	6
1.5.1. Sifa za Mwanachama anayestahili kupata mkopo.....	6
1.5.2. Sifa za Chama kinachostahili kupata mkopo .....	6
1.6. Aina ya Mikopo-BOSA .....	7
1.6.1. Mikopo ya Maendeleo.....	7
1.6.2. Mikopo wa Dharura.....	8
1.6.3. Mikopo wa Elimu.....	8
1.6.4. Mikopo wa Papo kwa Papo.....	9
1.7. Aina ya mikopo-FOSA .....	9
1.7.1 Mikopo wa Boresha Maisha .....	10
1.7.2 Mikopo wa Chipukizi.....	10
1.7.3 Mikopo wa Niwezeshe .....	10
1.7.4 Mikopo wa Ujasiriamali.....	11
1.7.5 Mikopo wa Wekeza .....	11
1.7.6 Mikopo wa Somesha (Somesha Loan).....	12
1.7.7 Mikopo wa Likizo (FOSA Festival Loan).....	12
1.7.8 Mikopo wa Matibabu (Matibabu Loan).....	13
1.7.9 Mikopo wa Bima (Insurance Loan) .....	13
1.7.9.1 Bima ya Afya.....	13
1.7.9.1 Bima ya Gari .....	13
1.7.10 Mikopo wa Usafiri.....	13
1.7.11 Mikopo wa Vifaa vya Nyumbani na Kielekroniki .....	14
1.7.12 Mikopo wa Washirika ( <i>Washirika Loan</i> ).....	14
1.8. Mfumo wa Utoaji Mikopo.....	15
1.9. Udhamini .....	16
1.10. Masharti ya Mikopo.....	17
1.11. Adhabu kwa Ukiukwaji wa Masharti ya Mikopo.....	18
SEHEMU YA PILI.....	20
2. SERA YA UFUATILIAJI NA MATENGO YA MIKOPO MIBAYA.....	20
2.1. Kurejesha Mikopo.....	20
2.2. Ufuatiliaji wa Marejesho ya Mikopo.....	20
2.3. Marejesho ya mikopo iliyochelewa.....	20
2.4. Madeni Mabaya .....	21
2.5. Kinga ya Madeni Mabaya.....	21
2.6. Kusimamisha Mikopo kwa Muda .....	21

2.7. Ucheleweshaji wa Mikopo .....	21
2.8. Mikopo iliyocheleweshwa na Mwanachama .....	22
2.9. Ukokotoaji na uainishaji mikopo iliyocheleweshwa .....	23
2.10. Matengo ya mikopo iliyocheleweshwa chamani .....	23
2.11. Mapitio ya potifolio ya mikopo na ukusanyaji wa mikopo iliyocheleweshwa.....	24
2.12. Mapato tarajiwa kutokana na uwepo wa mikopo iliyocheleweshwa....	25
2.13. Mapitio ya kufanya marekebisho ya mkopo .....	25
SEHEMU YA TATU .....	26
3. SERA YA UFUTAJI WA MIKOPO YA WANACHAMA .....	26
4. MENGINEYO.....	27
5. UTARATIBU WA MIKOPO.....	28
5.1. MKOPO WA MAENDELEO.....	28
5.2. MKOPO WA UJASILIAMALI.....	29
6. MAJINA YA WADHAMINI ISHIRINI (20) WALIOTIA SAINI ZAO KWA NIABA YA WANACHAMA WENZAO.....	31

## UTANGULIZI

Sera hii ya Mikopo imeandaliwa ili kuweka wazi taratibu za ukopeshaji wanachama na vilevile kukidhi matarajio ya wakopaji ambao ni wanachama waliokusanya nguvu zao pamoja kwa lengo la kupambana na umasikini. Sera ya mikopo ni utaratibu unaoandaliwa kuweka ukomo na uwiano wa kukopesha wanachama kwa kuzingatia Sheria, Kanuni za Ushirika, nyaraka za Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Masharti ya Chama.

**Bodi** ya Chama imepewa uwezo wa kutengeneza sera ili kuongoza kwa ufanisi zoezi zima la ukopeshaji na kuhakikisha mikopo inayotolewa inazingatia uwezo wa mkopaji na marejesho ya mikopo yanafanyika kwa wakati na kwa kuzingatia mkataba uliosainiwa. Kanuni za Ushirika zimeeleza kuwepo kwa Kamati ya Mikopo ambayo itasimamia kwa niaba ya Bodi utoaji mikopo kwa kuzingatia sera hii, na kwamba Bodi kupitia kamati ya Mikopo inaweza kukasimu utoaji wa baadhi ya mikopo kwa kamati ya utaalumu. (Technical committee).

**Kamati ya Mikopo** haina budi kuzingatia sera hii na kufanya kile kilichokusudiwa na Bodi ya Chama, ikiwa ni pamoja na kutayarisha mihtasari ya vikao vyake na kuwasilisha kwa Bodi ya Chama.

**Kamati ya Usimamizi** itasimamia sera ya mikopo kwa kutathmini maamuzi ya Kamati ya Mikopo na kamati ya kitaalam juu ya maombi mbalimbali ya mikopo ya wanachama na kuona kama mikopo iliyotolewa imezingatia matakwa ya sera hii. Kamati ya Usimamizi itaishauri Bodi pamoja na kuhakikisha ya kwamba mikopo yote iliyotolewa inarejeshwa.

Kamati ya Mikopo kwa kufuata sera hii itatumia utaratibu wa "FIFO" (first in first out) katika kutoa mikopo kwa wanachama. Hii ina maana kuwa maombi yaliyoletwa mwanzo ndio yatashughulikiwa kwanza. Kwa hiyo maombi yote

yatawekewa muhuri wenye tarehe ya kurudisha fomu na mwanachama atakuwa na haki ya kujulishwa idadi ya maombi yaliyokwisha pokelewa akipenda.

Sera hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu ambazo ni utoaji wa Mikopo, ufuatiliaji na matengo ya mikopo mibaya pamoja na ufutaji wa madeni mabaya. Kwa mujibu wa Kanuni za Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo za Mwaka 2014, Chama kinatakiwa kuandaa sera tatu za Mikopo ila Bodi ya Chama imependekeza kuandaa sera moja ambayo itahuisha maeneo yote muhimu yaliyoelekezwa na Kanuni kwa ajili ya kuwa na mtiririko mzuri (*Chronological order*) wa kuhifadhi kumbukumbu za Chama. Aidha, utaratibu huu utasaidia kuweka mpangilio mzuri unaotakiwa kutekelezwa na Kamati ya Mikopo au Afisa yeyote pasipo kuwa na shida ya kutafuta nyaraka husika sehemu nyingine.

## **SEHEMU YA KWANZA**

### **1. SERA YA MIKOPO**

#### **1.1. Utangulizi**

Sera ya mikopo ya TANESCO SACCOS ni mwongozo uliowekwa na Chama kwa ajili ya kusimamia namna ya utoaji wa mikopo ndani ya Chama. Taratibu hizi za mikopo zimetungwa kwa kufikiria misingi ya kanuni za utendaji bora wa Chama na lazima zifuatwe na kutumika katika shughuli zote za utoaji mikopo kwa wanachama. Sera hii itazingatia matakwa ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya Mwaka 2013, Kanuni za Vyama vya Ushirika za Mwaka 2015 pamoja na Kanuni za Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo za Mwaka 2014.

#### **1.2. Madhumuni ya Sera ya Mikopo**

- (a) Kuweka misingi na kanuni bora za utoaji mikopo
- (b) Kuepusha migongano isiyo ya lazima katika kutoa mikopo
- (c) Kupunguza hatari ya mikopo mibaya
- (d) Kujenga imani kwa taasisi za ndani na nje, wanachama na wananchi kwa ujumla.
- (e) Kuonyesha umakini wa Bodi katika kusimamia shughuli za Chama.

#### **1.3. Walengwa wa Sera hii**

##### **(a) Wadau wa ndani**

- (i) Wanachama ndio walengwa wakuu wa Sera hii kwa kuwa ndio wakopaji
- (ii) Wafanyakazi/Watendaji – Hawa ni wataalamu wa kuchanganua na kutathmini mikopo inayoombwa na inayotolewa.
- (iii) Viongozi/Kamati ya kitaalamu/Kamati ya mikopo – watahusika katika kusimamia na kuhakikisha kuwa taratibu zote za Sera zinafuatwa

**(b) Wadau wa nje**

- i) Wakaguzi wa nje – Watatumia Sera hii wakati wa ukaguzi.
- ii) Afisa ushirika – Ni mshauri katika utekelezaji wa sera hii kama mwakilishi wa Serikali.
- iii) Taasisi za Kifedha na wakopeshaji wengine – Chama kitakopa toka taasisi za kifedha pamoja na wakopeshaji wengine kulingana na taratibu za sera hii pamoja na Sera ya Usimamizi wa Ukwasi, Mali na Dhima.
- iv) Wakopaji wa nje - Chama kinaweza kukopesha Chama kingine kwa mujibu sheria na taratibu.
- v) Mrajis wa Vyama vya Ushirika – anahusika na kuidhinisha sera hii na kusimamia utekelezaji wake.

**1.4. Misingi ya Utoaji wa Mikopo kwa Wanachama**

**A. MTAJI (CAPITAL)**

Akiba na hisa za hiari za mwanachama zilizowekwa ndani ya Chama zitazingatiwa na kuwa kigezo muhimu cha kutoa mkopo kwa mwanachama

**B. TABIA (CHARACTER)**

Tabia ya mkopaji lazima itathiminiwe kulingana na ubora wake binafsi na kumbukumbu zake za mikopo. Wanachama, Kamati ya Usimamizi, Kamati ya mikopo au kiongozi yeyote wa chama anayemfahamu mkopaji anaweza kufanya tathmini ya tabia yake katika kurejesha mikopo. Dhamana kubwa iliyopita kiwango cha mkopo isiwe kigezo cha kumpa mkopo mwanachama asiyekuwa na tabia nzuri ya urejeshaji. Wakopaji wapya watatathiminiwa kwa kuzingatia uwezo wao wa Akiba/dhamana.

Kwa upande wa Vyama (mkopaji), Chama kitaangatia matakwa yote ya kisheria.

### C. HALI (CONDITION)

Hali ya utoaji wa mkopo kwa mwanachama itazingatia mambo ya nje yanayoathiri mkopo wa mwombaji

- i. Hali ya uchumi wa nchi
- ii. Thamani ya fedha
- iii. Sheria za nchi
- iv. Hali ya soko la biashara inayoombewa mkopo
- v. Hali ya soko la kazi/ajira
- vi. Na mambo mengine yanayoathiri hali ya urejeshaji wa mkopo

### D. UWEZO WA MTIRIRIKO WA KIFEDHA.

Uwezo wa kurejesha mkopo ndio kitu cha kwanza cha msingi cha kuangalia katika kutathimini uwezo wa mwanachama kurejesha mkopo anaomba. Katika kuchanganua uwezo wa kurejesha mkopo, vitu vitatu vifuatavyo vitazingatiwa;

- (i) **Uwezo uliopo hivi sasa wa kurejesha mkopo** - Uwezo alionao mwanachama wakati wa kufanya marejesho kwa mkopo aliopewa, utazingatiwa.
- (ii) **Uwezo na matarajio ya kupata** – Uwezo alionao mwanachama kupanga utaratibu wa kufanya marejesho kwa mkopo aliopewa utaangaliwa na kuzingatiwa. Chama kitatilia maanani uimara wa ajira na kipato cha familia. Aidha, Ajira mpya na za muda mfupi zitachukuliwa kuwa ina athari kubwa.
- (iii) **Hali ya kifedha** – Huu ni uwezo alionao mwanachama kutimiza wajibu wake.

### E. DHAMANA YA MKOPO (COLLATERAL)

Dhamana itakayowekwa/zitakazowekwa na mwanachama wakati wa kuomba mkopo zitatakiwa kuwa na thamani zaidi ya kiwango cha



mkopo utakaombwa. Aidha, tathmini halisi ya thamani ya dhamana itakayowekwa na wanachama itatakiwa kutathiminiwa vizuri kabla ya kuwekwa kwenye dhamana ya mkopo.

## **1.5. Taratibu za Utoaji Mikopo**

### **1.5.1. Sifa za Mwanachama anayestahili kupata mkopo**

- (a) Awe mwanachama wa TANESCO SACCOS anayechangia Akiba yake kila mwezi, Mwenye Hisa zisizopungua sabini na sita (76) na zenye thamani ya Tshs. 380,000 na anayekubali kufuata masharti ya mkopo;
- (b) Angalau mwanachama awe na muda katika Chama usiopungua miezi mitatu (3);
- (c) Asiwe na deni aliloshindwa kulipa ndani ya Chama na kwenye taasisi nyingine

### **1.5.2. Sifa za Chama kinachostahili kupata mkopo**

- (a) Chama kiwe na usajili kamili na kuwa kinaendesha shughuli zake kwa mujibu wa sheria (Chama hai).
- (b) Chama kiwe kimesajiliwa na kupatiwa leseni na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania
- (c) Chama kiwe na anuani.
- (d) Chama kiwe na taarifa ya hesabu zilizokaguliwa kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita na Shirika la ukaguzi na usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO).
- (e) Chama kiwe na ukomo wa madeni uliidhinishwa na Mkutano Mkuu wa Chama kwa mujibu wa sheria.

## **1.6. Aina ya Mikopo-BOSA**

### **1.6.1. Mikopo ya Maendeleo**

Mkopo huu utatolewa kulingana na akiba za mwanachama na utakopeshwa kwa madhumuni ya kufanikisha shughuli za kimaendeleo.

- a. Mwanachama ana uhuru wa kukopa kiwango ambacho hakizidi mara nne (4) ya akiba alizonazo katika Chama bila kuathiri kifungu namba 66(2 na 3) cha kanuni za SACCOS.
- b. Kiwango cha juu cha mkopo kitategemea uwezo wa mshahara wa mwanachama husika.
- c. Muda wa juu wa marejesho ya mkopo ni miezi sitini (60)
- d. Mwanachama ataruhusiwa kukopa tena iwapo atakuwa amemaliza mkopo wa awali, au amerejesha moja ya tatu (1/3) la deni la awali.
- e. Mwanachama ataruhusiwa kutunisha akiba zake kwa kuingiza fedha taslim katika akaunti ya Chama na atakuwa na haki ya kukopeshwa kutokana na akiba yake hiyo miezi miwili baada ya kutunisha akiba yake.
- f. Riba kwa mkopo wa maendeleo ni asilimia 1.0 kwa mwezi kwa baki ya mkopo (*Reducing Balance Method*)
- g. Mkopo huu una kinga ya bima ambayo italipwa na mkopaji.
- h. Mkopo huu hautatolewa iwapo baki ya mshahara wa mwanachama itakuwa chini ya theluthi moja (1/3)

- i. Mwanachama anayepitishia pensheni yake ya mwezi kwenye akaunti ya FOSA ataruhusiwa kukopa mara nne ya akiba zake na kurejesha kwa mujibu na matakwa sera hii.
- j. Mwanachama asiyepitisha pensheni yake ya mwezi kwenye akaunti ya FOSA ataruhusiwa kukopa mkopo huu kwa kiwango cha asilimia 100 ya akiba zake. Muda wa marejesho na riba zitakuwa kama zilivyoanishwa katika kipengele (c) na (f). Mkopo wa kwanza hautakuwa na wadhamini. Mkopo wa pili (mara mbili ya akiba) utakuwa na wadhamini na dhamana nyinginezo kama taratibu kama zilivyoainishwa katika kifungu namba 1.8
- k. Mkopo huu utatakiwa kuwa na dhamana kamilifu na kutafuta utaratibu kama utakavyobainishwa na Chama kwa wakati tofauti.

#### **1.6.2. Mkopo wa Dharura**

- a. Mkopo huu utatolewa kwa wanachama kwa kiwango cha kuanzia Tshs. 300,000.00 hadi Tshs. 3,000,000.00 na itategemea zaidi uwezo wa mshahara wa mwanachama na akiba alizonazo katika Chama
- b. Mkopo wa dharura hautatolewa kwa mwanachama ambaye atakuwa bado hajamaliza mkopo wa awali.
- c. Makato kwa mkopo ya dharura yatafanyika kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili.
- d. Riba kwa mikopo ya dharura itakuwa asilimia 2 kwa mwezi kwa baki ya mkopo.

#### **1.6.3. Mkopo wa Elimu.**

- a. Kiwango cha mkopo wa Elimu hakitazidi mara mbili ya mshahara wa mwanachama-
- b. Riba ya mkopo wa Elimu ni asilimia tano (5%) ya kiwango cha mkopo.

- c. Makato kwa mkopo wa Elimu yatafanyika kwa kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili.
- d. Mwanachama atalazimika kuwa na barua ya madai ya shule ambayo anatarajia kulipa ada yake mwenyewe, mtoto au mtegemezi wake.
- e. Mwanachama atakayekopa mkopo na kulipa kupitia pensheni ya mwezi atakopa mkopo huu mara moja au mbili ya pensheni yake ya mwezi na kuulipa ndani ya kipindi kisichozidi miezi kumi na mbili.
- f. Mkopo wa Elimu hautatolewa kwa mwanachama ambae atakuwa bado hajamaliza mkopo wa awali.

#### **1.6.4. Mkopo wa Papo kwa Papo**

- a. Utatolewa kwa kiwango cha kuanzia Tshs. 50,000.00 hadi Tshs. 300,000.00 kuanzia tarehe 10 hadi 20 ya kila mwezi.
- b. Makato ya marejesho ya mkopo huu yatafanyika mwezi unaofuata kwa mkupuo mmoja.
- c. Riba ya mkopo wa papo kwa hapo ni asilimia 10.
- d. Mwanachama ambaye hatarejesha mkopo huu kwa wakati, hatastahili kupewa mkopo mwingine mpaka atakapokuwa amerejesha mkopo wa awali.

Tanbihi: Mwanachama wa kundi la waajiriwa wa muda (temporary employees) atanufaika na bidhaa zote za Chama na atapaswa kulipa mkopo huo ndani ya muda wa mkataba uliosalia.

#### **1.7. Aina ya mikopo-FOSA**

Mikopo yote ya FOSA itatolewa kwa wanachama ambao mishahara yao inapitia kwenye akaunti zao za FOSA, isipokuwa mkopo wa ujasirimali. Mwanachama atawajibika kuhakikisha mishahara wake unapita katika akaunti yake ya FOSA

### 1.7.1 Mkopo wa Boresha Maisha

- a. Mwanachama ana uhuru wa kukopa kiwango ambacho hakizidi mara tano (5) ya mshahara halisi wa mwezi. Kiwango cha juu cha mkopo kitakuwa Tshs. milioni ishirini.
- b. Riba ya mkopo huu itakuwa asilimia 1.2 kwa mwezi kwa baki ya mkopo (*Reducing Balance Method*).
- c. Muda wa juu wa marejesho ya mkopo ni miezi sitini (60)
- d. Mwanachama ataruhusiwa kukopa tena iwapo atakuwa amemaliza mkopo wa awali, au amerejesha nusu ( $1/2$ ) ya deni la awali.
- e. Mwajiri/Mfuko wa hifadhi ya jamii utakuwa mdhamini wa mkopo huu kwa kuhakikisha mshahara/pensheni wa mfanyakazi/mwanachama unapita katika akaunti ya mwanachama ndani ya Chama.

### 1.7.2 Mkopo wa Chipukizi

- a. Mkopo huu utatolewa kwa Mwanachama ambaye ameajiriwa ndani ya kipindi cha miezi kumi na mbili au Mwanachama ambaye ana mkataba wa muda maalum usiopungua miezi kumi na mbili (12)
- b. Mwanachama anaweza kukopa kiwango ambacho hakizidi mara tano (5) ya mshahara halisi wa mwezi.
- c. Riba ya mkopo huu itakuwa asilimia 1.3 kwa mwezi kwa baki ya mkopo (*Reducing Balance Method*)

Muda wa juu wa marejesho ya mkopo ni miezi ishirini na nne (24) kwa wafanyakazi wa kudumu na miezi kumi na mbili (12) kwa wafanyakazi wa mkataba wa muda maalum.

### 1.7.3 Mkopo wa Niwezeshe

- a. Mwanachama anaweza kukopa kiwango kuanzia asilimia 10 hadi 25 ya mshahara halisi wa mwezi.
- b. Riba ya mkopo huu itakuwa asilimia 10 kwa mwezi kwa kiasi cha mkopo.
- c. Mkopo huu utarejeshwa mwezi unaofuata

- d. Mwajiri atakuwa mdhamini wa mkopo huu kwa kuhakikisha mshahara wa mfanyakazi unapita katika akaunti ya mwanachama ndani ya Chama.

#### 1.7.4 Mkopo wa Ujasiriamali

- a. Mwanachama anaweza kukopa kiwango kisichozidi Tshs. 10,000,000.00
- b. Riba ya mkopo huu itakuwa asilimia 1.375 kwa mwezi kiasi cha mkopo.
- c. Muda wa juu wa marejesho ya mkopo ni miezi ishirini na nne (24).
- d. Dhamana za mkopo huu zitakazokubalika ni pamoja na hati ya nyumba, kiwanja, hati ya shamba, au kadi halisi ya gari.
- e. Pamoja na masharti ya kipengele (d) mwanachama atatakiwa kuwasilisha: Mpango wa biashara (lazima), leseni ya biashara, usajili wa biashara (*business name*) na namba ya utambulisho wa mlipa kodi (kama biashara hiyo imesajiliwa).
- f. Mwanachama atatathimiwa kwa kigezo cha kufanya miamala katika akaunti yake ndani ya Chama angalau mara tatu kwa mwezi.
- g. Marejesho ya mkopo huu yataanza baada ya miezi mitatu (3) kupitia akaunti yake ya FOSA. Mwanachama atahakikisha akaunti yake ya FOSA inakuwa na salio tarehe ya marejesho.
- h. Iwapo marejesho ya mkopo huu yatacheleweshwa kwa zaidi ya siku 30, tozo ya asilimia 10 ya rejesho la mwezi itatozwa na kujumuishwa katika baki ya deni.

#### 1.7.5 Mkopo wa Wekeza

- a. Mwanachama anaweza kukopa mpaka mara mbili (2) ya kiasi cha hisa za hiyari alizoweka katika Chama.
- b. Riba ya mkopo huu itakuwa asilimia 8 kwa mwaka (*flat rate*)
- c. Mwanachama ataruhusiwa kukopa tena iwapo atakuwa amemaliza mkopo wa awali.
- d. Marejesho ya mkopo huu yatafanyika ndani ya miezi kumi na mbili (12)

- e. Marejesho ya Mkopo huu yatafanyika kupitia Akaunti yake ya FOSA.
- f. Iwapo marejesho ya mkopo huu yatacheleweshwa kwa zaidi ya siku 30, tozo ya asilimia 10 ya rejesho la mwezi itatozwa. Tozo hii pamoja na rejesho husika vitakatwa kwenye akaunti ya amana ya Hisa za Hiyari.

Tanbihi: Mwanachama wa kundi la waajiriwa wa muda (temporary employees) atanufaika na bidhaa zote za Chama na atapaswa kulipa mkopo huo ndani ya muda wa mkataba uliosalia.

#### **1.7.6 Mkopo wa Somesha (Somesha Loan)**

- a. Mwanachama anayepitisha mshahara wake FOSA anaweza kukopa mara mbili (2) ya amana ya elimu.
- b. Riba ya mkopo huu itakuwa asilimia 8 kwa mwaka (*flat rate*)
- c. Marejesho ya mkopo huu yatafanyika ndani ya miezi kumi na mbili (12)
- d. Marejesho ya Mkopo huu yatafanyika kupitia Akaunti yake ya FOSA. Iwapo marejesho ya mkopo huu yatacheleweshwa kwa zaidi ya siku 30, tozo ya asilimia 10 ya rejesho itatozwa na kujumuishwa katika baki ya deni. Tozo hii pamoja na rejesho husika vitakatwa kwenye akaunti ya amana ya Elimu.

#### **1.7.7 Mkopo wa Likizo (FOSA Festival Loan)**

- a. Mwanachama anaweza kukopa mara mbili (2) ya amana ya Likizo
- b. Riba ya mkopo huu itakuwa asilimia 8 kwa mwaka (*flat rate*)
- c. Marejesho ya mkopo huu yatafanyika ndani ya muda wa miezi kumi na mbili (12)
- d. Marejesho ya Mkopo huu yatafanyika kupitia Akaunti yake ya FOSA. Iwapo marejesho ya mkopo huu yatacheleweshwa kwa zaidi ya siku 30, tozo ya asilimia 10 ya rejesho itatozwa na kujumuishwa katika baki ya deni. Tozo hii pamoja na rejesho husika vitakatwa kwenye akaunti ya amana ya Likizo

### **1.7.8 Mkopo wa Matibabu (Matibabu Loan)**

- a. Mwanachama anaweza kukopa mara mbili (2) ya amana ya Matibabu
- b. Riba ya mkopo huu itakuwa asilimia 8 kwa mwaka (*flat rate*)
- c. Marejesho ya mkopo huu yatafanyika ndani ya muda wa miezi kumi na mbili (12)
- e. Marejesho ya Mkopo huu yatafanyika kupitia Akaunti yake ya FOSA. Iwapo marejesho ya mkopo huu yatacheleweshwa kwa zaidi ya siku 30, tozo ya asilimia 10 ya rejesho itatozwa na kujumuishwa katika baki ya deni. Tozo hii pamoja na rejesho husika vitakatwa kwenye akaunti ya amana ya Matibabu.

### **1.7.9 Mkopo wa Bima (Insurance Loan)**

#### **1.7.9.1 Bima ya Afya**

- a. Mwanachama anaweza kuomba mkopo wa Bima ya afya kulingana na idadi ya wanufaika. Idadi ya juu ya wategemezi itakuwa ni watano.
- b. Marejesho ya mkopo huu yatafanyika ndani ya muda wa miezi kumi na mbili (12)

#### **1.7.9.1 Bima ya Gari**

- a. Mwanachama anaweza kuomba mkopo wa bima ya gari kulingana na thamani ya gari yake. Bima hii inaweza kuwa bima kubwa (*comprehensive*) au bima ndogo (*third party*)
- b. Marejesho ya mkopo huu yatafanyika ndani ya muda wa miezi kumi na mbili (12)

Kwa mikopo hii ya bima, Chama kitatoza tozo ya shilingi elfu hamsini (Tshs. 50,000) kwa kila mkopo.

### **1.7.10 Mkopo wa Usafiri**



- a. Mwanachama anaweza kukopa chombo cha usafiri kupitia mawakala waliosajiliwa na Chama kwa kiwango kisichozidi shilingi milioni hamsini (Tshs. 50,000,000)
- b. Riba ya mkopo huu itakuwa asilimia 9.6 kwa mwaka (*reducing balance*)
- c. Marejesho ya mkopo huu yatafanyika ndani ya miezi thelathini na sita (36)
- d. Marejesho ya Mkopo huu yatafanyika kupitia Akaunti yake ya FOSA.
- e. Chama kitashikilia hati halisi ya umiliki wa gari mpaka Mwanachama atakapo maliza deni. Hati hii itakuwa dhamana ya Mkopo huu.
- f. Kwa kipindi chote cha mkopo huu, gari litakatiwa bima kubwa.

#### 1.7.11 Mkopo wa Vifaa vya Nyumbani na Kielekroniki

- a. Mwanachama anaweza kukopa kifaa cha nyumbani au kielekroniki kupitia wakala/watoa huduma walioingia mkataba na Chama. Kiwango cha juu cha mkopo huu hakitazidi shilingi milioni tano (Tshs. 5,000,000)
- b. Riba ya mkopo huu itakuwa asilimia 1.4 kwa mwezi (*reducing balance*)
- c. Marejesho ya mkopo huu yatafanyika ndani ya miezi kumi na mbili (12)
- d. Marejesho ya Mkopo huu yatafanyika kupitia Akaunti yake ya FOSA.

#### 1.7.12 Mkopo wa Washirika (*Washirika Loan*)

- a. Chama kinaweza kukopesha Chama cha Ushirika wa akiba na mikopo mpaka kiasi cha shilingi bilioni moja (Tshs. 1,000,000,000)
- b. Riba ya mkopo huu itakuwa asilimia 1.0 kwa mwezi (*reducing balance*)
- c. Marejesho ya mkopo huu yatafanyika ndani ya miezi thelathini na sita (36)
- d. Marejesho ya Mkopo huu yatafanyika kwa njia za kuwasilisha hundi, au kufanya miamala ya kielekroniki na kuingiza moja kwa moja kwa Chama (TISS).
- e. Chama (taasisi) kitatakiwa kufungua akaunti ya FOSA ili kuruhusu kufanyika kwa miamala.

### **1.8. Mfumo wa Utoaji Mikopo.**

- a.** Mwanachama anayestahili kuomba mkopo ni lazima awe ametimiza miezi mitatu tangu alipojiunga na Chama na awe amelipa asilimia 50 ya hisa za lazima.
- b.** Mwanachama anapodhamiria kuchukua mkopo atajaza fomu husika ya maombi ya mkopo, akielezea bayana madhumuni ya mkopo anaotaka kuchukua.
- c.** Mikopo yote itakingwa kwa kutumia dhamana zilizo ndani ya Chama (akiba, hisa za hiari na amana za muda maalum), na/au hati halisi ya mali zisizohamishika.
- d.** Mkopo utadhaminiwa kwa ukamilifu na mwanachama mwenyewe au kudhaminiwa na wanachama wenzake.
- e.** Fomu za maombi ya mikopo zitapelekwa kwenye kamati ya mikopo ili kujadiliwa na hatimaye kukubaliwa au kukataliwa kwa kuzingatia sera ya mikopo iliyopo na wajumbe wa Kamati ya Mikopo.
- f.** Fomu za maombi ya mikopo yaliyokubaliwa zitatayarishiwa malipo na Mhasibu wa Chama na kukabidhiwa kwa wanachama baada ya utaratibu wa malipo kukamilika. Maombi yaliyokataliwa lazima yatolewe maelezo na kamati ya mikopo na sababu za kukataliwa maombi hayo.
- g.** Kamati ya mikopo inaweza kupunguza kiasi cha mkopo ulioombwa endapo itabaini kwamba mkopaji hana sifa za kupewa mkopo huo, ikiwemo ile ya bakaa ndogo ya mshahara 'net pay', akiba pungufu, kudaiwa na taasisi mbalimbali za fedha.
- h.** Mikopo ya Elimu, Dharura na Papo kwa papo itatolewa na kuidhinishwa na kamati ya kitalaam kwa kuzingatia uwezo wa mkopaji kulipa mkopo huo na

taarifa ya mikopo ilizopitishwa itapelekwa kwenye kikao cha kamati ya mikopo kwa uhakiki.

- i. Iwapo mwanachama atahitaji kuongeza akiba zake kupitia benki/fedha taslim kwa lengo la kukopea atalazimika kupata idhini ya kamati ya mikopo au Meneja kabla hajaingiza fedha zake ili kuona kama Chama kina uwezo wa kumkopesha.
- j. Kwa wanachama wenye mikataba ya muda maalum, iwapo watahitaji mkopo ambao makato yake yanazidi kipindi kilichobaki cha ajira atatakiwa kuwasilisha barua ya mwajiri inayothibitisha kuongeza au kutarajia kuongeza kipindi cha mkataba kwa awamu nyingine.
- k. Kamati ya mikopo itakuwa na maamuzi ya mwisho juu ya kumpa mkopo mwanachama kwa kuzingatia:
  - I. Taratibu za Chama za mikopo
  - II. Maelezo ya mwanachama binafsi.
  - III. Tabia ya mwanachama ikiwa pamoja na uaminifu.
  - IV. Uwezo wa mkopaji kulipa mikopo atakayopewa na Chama.

### **1.9. Udhamini**

- a. Mwanachama anayestahili kuwa mdhamini wa mkopo ni lazima awe ametimiza mwaka mmoja tangu alipojiunga na Chama.
- b. Dhamana zilizokataliwa lazima zitolewe maelezo na Kamati ya Mikopo na sababu za kukataliwa dhamana hizo.
- c. Kamati ya Mikopo inaweza kupunguza kiasi cha mkopo ulioombwa endapo itabaini kwamba dhamana za mkopaji hazina sifa ya kupewa mkopo huo. Dhamana ya nyumba ya familia lazima ipate ridhaa ya pande zote mbili.

- d. Kwa Mkopo wa maendeleo/Ujasiriamali, iwapo dhamana ya mkopo itakuwa Shamba/Kiwanja/Nyumba/Gari, mwanachama atawajibika kuthaminisha mali hiyo kwa wathamini walioidhinishwa na Chama.
- e. Kwa Mkopo wa maendeleo/Ujasiriamali, iwapo dhamana ya mkopo itakuwa Shamba/Kiwanja/Nyumba; mwenza wa mkopaji atathibitisha kuridhia mali hiyo kutumika kama dhamana ya mkopo husika.
- f. Mkopaji atatakiwa kuwasilisha kwenye Chama, hati halisi ya shamba/kiwanja/nyumba iliyowekwa rehani baada ya uhakiki kufanyika
- g. Iwapo dhamana ya mkopo huu ni gari, mkopaji atatakiwa kuwasilisha kwenye Chama, hati halisi ya gari iliyowekwa rehani.
- h. Chama kitarejesha dhamana iliyowekwa rehani baada ya maresho ya mkopo kukamilika

#### **1.10. Masharti ya Mikopo**

- a. Kazi ya kutoa mikopo itafanywa na Kamati ya Mikopo pekee. Viongozi wa Bodi na kamati ya usimamizi wataashauri pale itakapokuwa lazima kufanya hivyo katika vikao halali vya Bodi au kamati ya usimamizi. Bodi inaweza kukasimu baadhi ya majukumu ya utoaji mikopo kwa Meneja wa Chama.
- b. Mwanachama ana haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa Kamati ya Mikopo kwa kuandika barua kwa Mwenyekiti wa Chama iwapo ataona hakutendewa haki na kamati hiyo. Mwenyekiti ataiwasilisha kwenye Bodi kwa ajili ya kujadiliwa na kutolewa uamuzi.
- c. Wakati wa kusikiliza rufaa hiyo wajumbe wa Kamati ya Mikopo hawatapiga kura.
- d. Hairuhusiwi kwa mwanachama kufidia mkopo kwa kutumia akiba zake zilizopo katika Chama ila kama atakuwa amejitoa uanachama.

- e. Mwanachama aliyekopa ataruhusiwa kuchukua mkopo mwingine wa Maendeleo kwa kulipa deni lake lote pamoja na adhabu ya kukatisha mkataba kwa kiwango kitakachokuwa kimepitishwa na Mkutano Mkuu.
- f. Mwanachama atalazimika kulipa deni pamoja na riba iwapo atakatisha mkataba kwa mikopo ya Dharura, Elimu na Papo kwa papo.
- g. Mwanachama ambaye kwa sababu yeyote ile ataomba likizo bila malipo atawajibika kuitaarifu ofisi jinsi atakavyolipa deni lake lote au kueleza kwa maandishi jinsi atakavyolipa deni hilo katika mkataba maalum na Chama.
- h. Mwanachama ambaye ataondoka na deni la Chama bila kuitarifu ofisi, Chama kitachukua hatua zifuatazo:
  - i. Kufidia mkopo kwa kutumia akiba zake zilizopo katika Chama.
  - ii. Kuwaarifu wadhamini wake juu ya kuwajibika kwao kulipa deni la Mwanachama husika kwa kupitia akiba zao.
  - iii. Ofisi itawasiliana na mwajiri wake mpya juu ya deni analodaiwa na Chama iwapo atakuwa ameajiriwa.
- i. Mwanachama aliyesimamishwa kazi hataruhusiwa kukopa mkopo unaozidi akiba zake katika Chama.
- j. Kamati ya mikopo itaidhinisha mikopo kwa kuangalia vigezo kama umri na muda kuisha kwa mkataba wa kazi.

#### **1.11. Adhabu kwa Ukiukwaji wa Masharti ya Mikopo.**

- a. Mwanachama atakayetoa taarifa za uongo kwa madhumuni ya kujipatia mkopo ambao hastahili, atapewa adhabu ya kutokopeshwa mkopo wowote kwa kipindi cha miezi kumi na miwili (12) baada ya kumaliza mkopo, na

endapo atafanya kosa jingine kama hilo atasimamishwa uanachama na suala lake litapelekwa katika Mkutano Mkuu kwa uamuzi.

- b.** Mwanachama anatakiwa afuate utaratibu uliopo katika sera za mikopo za Chama za kudai haki yake. Kutumia lugha ya vitisho au matusi kwa viongozi au watumishi wa Chama ni kosa. Ikithibitika kwamba mwanachama husika amefanya vitendo hivi kwa nia ya kuwapaka matope viongozi au watumishi atasimamishwa uanachama na suala lake kufikishwa katika Mkutano Mkuu kwa uamuzi wa mwisho.
- c.** Endapo mwanachama kwa kutumia njia zisizokuwa halali atasitisha makato ya mkopo kutoka katika mshahara wake, au kukaa kimya bila kutoa taarifa, au kutoroka na deni la Chama, kitendo hiki kitachukuliwa kama utovu wa nidhamu na ukiukaji mkubwa wa mkataba. Bodi itamchukulia hatua za kinidhamu mwanachama wa aina hiyo kwa kumpa tozo ya kumuongezea asilimia 10% kwa kiasi cha makato aliyochelewesha au hatua kali zaidi za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake.
- d.** Mkopo ndiyo biashara inayoendeshwa na Chama, hivyo marejesho ya mikopo ndiyo yanawezesha Chama kupata faida. Kiongozi au mtumishi wa Chama atakayevuruga au kuchelewesha marejesho ya mkopo ataandikiwa barua ya onyo na kama atasababisha hasara kwa kipindi hicho atalazimishwa kufidia hasara hiyo, na siyo mkopaji wa mkopo huo.

## SEHEMU YA PILI

### 2. SERA YA UFUATILIAJI NA MATENGO YA MIKOPO MIBAYA

#### 2.1. Kurejesha Mikopo

- (a) Mwanachama atafanya marejesho ya mkopo pamoja na riba kwa kupitia akaunti ya Chama au fedha taslimu kwa utaratibu utakaowekwa na Chama.
- (b) Taarifa juu ya maendeleo ya mikopo zitaandaliwa na Kamati ya Mikopo na kuwasilishwa kwa Bodi ya Chama.

#### 2.2. Ufuatiliaji wa Marejesho ya Mkopo

- (a) Kila mwanachama ana wajibu wa kuhakikisha marejesho ya mikopo yake aliyochukua yanafanyika kama ilivyokubaliwa.
- (b) Kamati ya Mikopo/Meneja watahusika mara kwa mara kutengeneza taarifa ya hali halisi ya mikopo ya wanachama kila mwezi.
- (c) Taarifa zitaonyesha hali halisi ya maendeleo ya mikopo na zitawasilishwa mbele ya Bodi kila baada ya miezi mitatu.

#### 2.3. Marejesho ya mikopo iliyochelewa

- (a) Mikopo iliyochelewa ni mikopo ambayo haijalipwa katika muda uliopangwa kuanzia siku ya kwanza aliyotakiwa kulipa mikopo hiyo.
- (b) Mikopo iliyocheleweshwa na wanachama itatozwa adhabu kulingana na kiasi cha deni analodaiwa kwa muda huo.
- (c) Adhabu itakayotozwa kwa mwanachama aliyechelewa itakuwa kama ifuatavyo:
  - i. Kila mwezi atatozwa 10% ya kiasi cha rejesho alichotakiwa kurejesha

**TANBIHI:** Mwanachama anapewa siku tatu baada ya tarehe ya mwisho ya kurejesha mkopo kama siku za huruma kurejesha mkopo bila faini. Baada ya hapo atalazimika kulipa 10% ya mwezi wa kwanza kwa kuchelewesha. Baada ya siku thelathini adhabu itaendelea vivyo hivyo ikijuimusha fedha iliyotakiwa kurejeshwa bila kuwa na siku za huruma za kurejesha mkopo

#### **2.4. Madeni Mabaya**

- a. Madeni mabaya ni yale ambayo yatakuwa yameshindwa kurejeshwa katika kipindi cha miezi 12 na yasiyoweza kurejeshwa.
- b. Madeni mabaya yatafutwa katika mahesabu ya Chama yatakapokuwa yamefikia zaidi ya miezi kumi na mbili (12)
- c. Chama kitaendelea kufuatilia madeni hayo kwa kutumia wakala wa ukusanyaji madeni na gharama italipwa na mwanachama husika.

#### **2.5. Kinga ya Madeni Mabaya**

Chama kitatenga asilima 15% ya faida kila mwaka kwa ajili ya kulipia madeni mabaya.

#### **2.6. Kusimamisha Mikopo kwa Muda**

Chama kinaweza kusimamisha utoaji wa mikopo ya aina fulani kulingana na mwenendo wa ulipaji wa mikopo hiyo.

#### **2.7. Ucheleweshaji wa Mikopo**

Mikopo yote itakayotolewa na Chama kwa wanachama wake itatambulika kama imecheleweshwa iwapo muda wake wa marejesho utakuwa umepita pasipo kutolewa kwa taarifa yoyote. Sera hii itafanyiwa mapitio angalau kila mwaka ili kuboresha vigezo na taratibu zitakazosaidia kubaini mikopo iliyocheleweshwa. Marekebisho yatakayofanyika yataainisha angalau mambo yafuatayo:-



- (a) Muda ambapo ukusanyaji wa mikopo iliyocheleweshwa utaongezwa au kuhuishwa kwa ajili ya kusaidia wanachama;
- (b) Maelezo ya hatua mbalimbali za utaratibu wa kukusanya mikopo;
- (c) Vigezo na utaratibu wa kuidhinisha Mikopo hiyo pamoja na mamlaka zitakazohitajika kuongeza muda wa marejesho au kuunda upya mikopo.

## **2.8. Mikopo iliyocheleweshwa na Mwanachama**

Mikopo ya wanachama wa itatambuliwa kuwa imecheleweshwa kulipwa iwapo mambo yafuatayo yatabainika:-

- a. Iwapo malipo ya marejesho ya mwanachama yatakuwa pungufu ya malipo yaliyotakiwa kulipwa kwa mujibu wa masharti ya mkataba uliosainiwa na mwanachama kipindi anachukua mkopo.
- b. Endapo malipo ya marejesho ya mwanachama hayatafanyika ndani ya siku thelathini tangu marejesho hayo kutakiwa kufanyika bila kujali kuwa mkopo uliocheleweshwa ni riba tu au riba na mkopo msingi (Principal).
- c. Iwapo Jedwali la marejesho ya mkopo lililopo kwenye fomu ya mikopo halitazingatiwa katika marejesho ya mkopo ya mwanachama.
- d. Mkopo utatakiwa kutolewa taarifa kwamba umecheleweshwa baada ya kushindwa kufanyika kwa rejesho moja kamili bila kujali kuwa marejesho yanafanyika kwa siku, wiki, mwezi au kwa kipindi kirefu zaidi.
- e. Chama kitatayarisha taarifa ya mikopo iliyocheleweshwa ndani ya siku kumi na tano baada ya kuisha kipindi ambacho taarifa hiyo inahusika na kusainiwa na Afisa Mikopo wa Chama na kuwekwa ofisini kwa ajili kupitiwa na wanachama. Taarifa ya ucheleweshwaji wa mikopo itajumuisha mambo yafuatayo:-
  - i. Jina la mwanachama, anwani na mawasiliano yake binafsi;

- ii. Tarehe na masharti ya mkopo ulipotolewa;
- iii. Mkopo halisi uliotolewa na bakaa la deni linalodaiwa ambalo halijarejeshwa
- iv. Majina ya wadhamini na dhamana ya mkopo iliyowekwa; na
- v. Taarifa nyingine zinazohusika kwa mujibu wa fomu ya mkopo.

## **2.9. Ukokotoaji na uainishaji mikopo iliyocheleweshwa**

Chama kitakuwa kinafanya ukokotoaji wa mikopo iliyocheleweshwa kwa kuanzia tarehe ya mwisho ambayo rejesho la mkopo husika lilifanyika mpaka pale malipo yote yatakapokuwa yamekamilika. Mikopo iliyocheleweshwa itakokotolewa kila mwezi na kutolewa taarifa siku ya mwisho wa mwezi ambapo mikopo hiyo itaainishishwa katika makundi yafuatayo:-

- (a) *Mikopo iliyopo kwenye Angalizo* – marejesho ya mkopo msingi na au riba kuchelewa kwa siku 31 – 90;
- (b) *Mikopo iliyopo Chini ya kiwango* – marejesho ya mkopo msingi na au riba kuchelewa kwa siku 91 – 180;
- (c) *Mikopo yenye Mashaka* - marejesho ya mkopo msingi na au riba kuchelewa kati ya siku 181 - 365; na
- (d) *Mikopo Mibaya/Hasara* - Mikopo inayochukuliwa kuwa haiwezi kukusanywa au ni ya thamani ndogo ambayo haiwezi kuendelea kutambuliwa kama mali, na marejesho ya mkopo msingi au mkopo msingi na riba hayajakusanywa kwa zaidi ya siku 365.

## **2.10. Matengo ya mikopo iliyocheleweshwa chamani**

Chama kitatenga fedha zake kwa ajili ya kufidia kiasi cha mikopo mibaya iliyocheleweshwa na wanachama kwa kuzingatia kiwango halisi kilichocheleweshwa. Aidha, ili kufidia kiasi cha mikopo hiyo mibaya, matengo ya fedha hizo yatatengwa kama ifuatavyo:-

- (a) Kiasi cha 10% ya bakaa ya mkopo kwa mikopo iliyo katika kundi la angalizo;
- (b) Kiasi cha 30% ya bakaa ya mkopo kwa mikopo iliyo katika kundi la chini ya kiwango;
- (c) Kiasi cha 50% ya bakaa ya mkopo kwa mikopo iliyo katika kundi la Mikopo yenye mashaka; na
- (d) Kiasi cha 100% ya bakaa ya mkopo kwa mikopo iliyo katika kundi la mikopo mibaya/hasara.

Kiasi cha tengo litakalotengwa kwa ajili ya kufidia mikopo mibaya iliyocheleweshwa kitawekwa kwenye akaunti ya mikopo mibaya kwa kuzingatia matakwa ya kanuni za mpito.

#### **2.11. Mapitio ya potifolio ya mikopo na ukusanyaji wa mikopo iliyocheleweshwa**

Chama kitafanya mapitio ya potifolio ya mikopo yake angalau mara moja kwa kila robo mwaka, na kuhakikisha kuwa:

- (a) Ukopesaji unaendana na sera ya mikopo iliyo dhinishwa;
- (b) Akaunti za mikopo mibaya zitajulikana na kuainishwa vya kutosha kulingana na vigezo vya uainishaji vilivyomo katika kanuni hizi; na
- (c) Kiwango cha kutosha kwa ajili ya kufidia hasara inayoweza kutokea katika Chama kinatengwa na kutunzwa kwa wakati wote.
- (d) Iwapo mkopo utainishwa kama hasara, Chama kitafanya makusanyo kutoka katika hisa za hiari ambazo zimetumika kama dhamana kutoka kwa wadhamini na itaendelea kukusanya kutoka katika dhamana yoyote iliyowekwa.

- (e) Chama kitaajiri mkusanya madeni kukusanya madeni ya mikopo iliyocheleweshwa na ada kama ilivyoainishwa katika makubaliano ya mkopo.

Bila kuathiri maelekezo mengine hapo juu, mkusanyaji wa madeni atapaswa kupata ada yake moja kwa moja kutoka kwa mdaiwa.

### **2.12. Mapato tarajiwa kutokana na uwepo wa mikopo iliyocheleweshwa**

Chama kitasitisha riba zote tarajiwa ambazo zitakuwa zimekadiriwa kupatikana kwenye mwaka husika kutokana na mikopo iliyocheleweshwa iwapo mkopo uliotolewa hautalipwa kwa siku tisini. Aidha, Chama kitaondoa mapato tarajiwa yanayotokana na mikopo kutoka katika akaunti ya mapato tarajiwa. Chama kitahakikisha kwamba kiasi cha mapato tarajiwa katika mizania ya Chama hakitazidi wastani wa kiasi cha mapato ya riba ya mikopo kwa mwezi wa mwaka uliopita.

### **2.13. Mapitio ya kufanya marekebisho ya mkopo**

Chama hakitafanya marekebisho ya mkopo zaidi ya mara moja kwa wanachama wake watakaopewa mikopo na kushindwa kurejesha kwa wakati. Mkopo wowote ambao umefanyiwa marekebisho au mabadiliko katika masharti yake ya awali, hautapaswa kuainishwa kama “chini ya kiwango” isipokuwa kama marejesho ya mkopo huo yamefanyika kikamilifu mara sita mfululizo tangu mkopo ulipofanyiwa marekebisho. Aidha, iwapo mkopo huo utafanyiwa marejesho kikamilifu mara sita mfululizo, mkopo huo utaaainishwa kama mkopo usiocheleweshwa. Pia, Chama kitatakiwa kutoa taarifa ya mikopo yote iliyofanyiwa marekebisho kama taarifa inayojitegemea katika mizania ya hesabu zake. Iwapo chama kitafanya marekebisho hayo, hakipaswi kujumuisha riba ya mkopo utaofanyiwa marekebisho kwakuwa riba yake yote itakuwa imeshalipwa kabla ya mkopo husika kufanyiwa marekebisho.

## SEHEMU YA TATU

### 3. SERA YA UFUTAJI WA MIKOPO YA WANACHAMA

Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo TANESCO kitafuta mikopo yake kutoka katika mizania yake kama kanuni Na.79 ya Vyama vya Akiba na Mikopo ya mwaka 2014 inavyoelekeza endapo:

- (a) Mkopo utacheleishwa kurejeshwa kwa zaidi ya siku 365;
- (b) Chama kitapoteza haki zake za kimkataba zinazohusiana na mkopo husika;
- (c) Mkopo utakapoonekana hauwezi kukusanywa;
- (d) Hakuna uwezekano wa Chama kukusanya mkopo wake kutokana na hukumu ya mahakama.
- (e) Dhamana zote zimeshikiliwa, kutathminiwa na kuuzwa, na mapato yanayotokana na mauzo kushindwa kufikia kiwango chote cha mkopo kinachodaiwa,
- (f) Chama hakina uwezo wa kukusanya mkopo au hakuna dhamana au jitihada za kukusanya deni zimeshindikana.

**TANBIHI:** Iwapo mkopo wa mwanachama utafutwa na kama mwanachama huyo atakuwa hajatangazwa kufilisika, mkopo huo utapaswa kufuatiliwa na kukusanywa kama mikopo mingine. Aidha, taarifa za mikopo yote iliyofutwa zitapaswa kuwa siri ili kutoathiri urejeshwa wa mikopo kwa wakati kwa wakopaji wengine. Pia, Matengo yatapaswa kufanywa kwa mikopo na mali zote zenye matatizo.

#### 4. MENGINEYO

- (a) TANESCO SACCOS inaongozwa kwa kuzingatia Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 06 ya mwaka 2013 na Kanuni zake za mwaka 2014 na 2015 pamoja na Nyaraka za Mrajis, Masharti ya Chama na Sera za Chama.
- (b) Wanachama wa TANESCO SACCOS ndiyo walinzi wa taratibu zilizotajwa hapo juu, kwa kuzingatia sheria, kuwa wakweli na kutekeleza wajibu wao ili kuboresha huduma za Chama.
- (c) Bodi ya Chama imefanya kazi ya kuandaa Sera ya Mikopo, lakini haitakuwa na maana yeyote kama walengwa ambao ni wanachama hawataielewa na kuizingatia. Hivyo, haki ya kukopa aliyonayo mwanachama iendane na wajibu wa kuilinda sera hii ili iwe mwongozo wa shughuli za Chama.
- (d) Kwa kuwa sera ni kitu kinachobadilika, maoni ya wadau wa ndani na wa nje yanakaribishwa ili kuongeza wigo mpana zaidi wa mawazo.
- (e) Mabadiliko yeyote ya kiwango cha riba juu ya mkopo yataamuliwa na wajumbe wa Mkutano Mkuu wa mwaka.

## 5. UTARATIBU WA MIKOPO

### 5.1. MKOPO WA MAENDELEO

#### a) Utaratibu wa maombi

- i. Mwanachama atajaza fomu ya maombi ya mkopo wa Maendeleo (Fomu namba MM 01)
- ii. Iwapo dhamana ya mkopo huu itakuwa Shamba/Kiwanja/Nyumba/Gari, mwanachama atawajibika kuthaminisha mali hiyo kwa wathamini walioidhinishwa na Chama
- iii. Iwapo dhamana ya mkopo huu itakuwa Shamba/Kiwanja/Nyumba; mwenza wa mkopaji atathibitisha kuridhia mali hiyo kutumika kama dhamana ya mkopo kama ilivyo kwenye kipengele (A) 7. Iwapo mkopaji hatakuwa na mwenza, atatakiwa kujaza fomu ya Hati ya Kiapo cha Mkopaji asiye na Mwenza (Fomu namba MMU 01)
- iv. Baada ya kupokea fomu ya maombi ya mkopo, Chama kitafanya uhakiki wa dhamana iliyowekwa kwa kutumia Afisa/Mwakilishi wa Chama (Fomu namba MMU 02)
- v. Chama kitafanya uhakiki wa mali (*verification of title*) kwenye mamlaka husika (Fomu namba MMU 03)
- vi. Mkopaji atatakiwa kuwasilisha kwenye Chama, hati halisi ya shamba/kiwanja/nyumba iliyowekwa rehani baada ya uhakiki kufanyika
- vii. Chama kutoa hati ya kuthibitisha kupokea hati halisi ya dhamana (Fomu namba MMU 04)
- viii. Mkopo utatolewa baada ya kutathmini thamani ya mali iliyowekwa rehani (fomu namba MMU 05)
- ix. Iwapo dhamana ya mkopo huu ni Gari; mkopaji atatakiwa kujaza fomu ya Hati ya kudhaminisha Gari (Fomu namba MMU 06)
- x. Mkopaji atatakiwa kuwasilisha kwenye Chama, hati halisi ya Gari iliyowekwa rehani.
- xi. Chama kutoa hati ya kuthibitisha kupokea hati halisi ya dhamana (Fomu namba MMU 04)
- xii. Chama kitafanya usajili wa hati halisi ya dhamana kwa mamlaka husika (fomu namba MMU 07)
- xiii. Mkopo utatolewa
- xiv. Chama kitarejesha dhamana iliyowekwa rehani baada ya maresho ya mkopo kukamilika (Fomu namba MMU 08 na MMU 09)

b) Viambatanisho

- i. Hati ya Mshahara (payslip)
- ii. Nakala ya kitambulisho
- iii. Fomu ya Uhakiki wa dhamana ya mkopaji
- iv. Picha ya mkopaji na mwenza wakiwa mbele ya mali inayowekwa rehani
- v. Taarifa ya uthaminishaji wa mali (shamba/kiwanja/nyumba)
- vi. Hati ya kiapo cha kudhaminisha Gari (iambatane na 'cover note ya Bima 'comprehensive')
- vii. Hati ya kiapo cha mkopaji asiye na mwenza
- viii. Hati halisi ya mali ilyowekwa rehani

**Tanbihi:** Gari isizidi miaka 15 tangu ilipotengenezwa na isizidi cc 3,500.

5.2.           MKOPO WA UJASILIAMALI

a) Utaratibu wa maombi

- i. Mwanachama atajaza fomu ya maombi ya mkopo wa Ujasiriamali (Fomu namba MU 01)
- ii. Iwapo dhamana ya mkopo huu itakuwa Shamba/Kiwanja/Nyumba/Gari, mwanachama atawajibika kuthaminisha mali hiyo kwa wathamini walioidhinishwa na Chama
- iii. Iwapo dhamana ya mkopo huu itakuwa Shamba/Kiwanja/Nyumba; mwenza wa mkopaji atahibitisha kuridhia mali hiyo kutumika kama dhamana ya mkopo kama ilivyo kwenye kipengele F (1)(b). Iwapo mkopaji hatakuwa na mwenza, atatakiwa kujaza fomu ya Hati ya Kiapo Cha Mkopaji Asiye na Mwenza (Fomu namba MMU 01)
- iv. Baada ya kupokea fomu ya maombi ya mkopo, Chama kitafanya uhakiki wa dhamana iliyowekwa kwa kutumia Afisa/Mwakilishi wa Chama (Fomu namba MMU 02 au/na Fomu namba MU 02)
- v. Chama kitafanya uhakiki wa mali (verification of title) kwenye mamlaka husika (Fomu namba MMU 03)
- vi. Mkopaji atatakiwa kuwasilisha kwenye Chama, hati halisi ya shamba/kiwanja/nyumba iliyowekwa rehani baada ya uhakiki kufanyika



- vii. Chama kutoa hati ya kuthibitisha kupokea hati halisi ya dhamana (Fomu namba MMU 04)
- viii. Chama kitafanya usajili wa hati halisi ya dhamana kwa mamlaka husika
- ix. Mkopaji atajaza, kusaini na kurejesha hati ya ahadi (Fomu namba MU 03)
- x. Mkopo utatolewa baada ya kutathmini thamani ya mali iliyowekwa rehani (fomu namba MMU 05)
- xi. Iwapo dhamana ya mkopo huu ni Gari; mkopaji atatakiwa kujaza fomu ya Hati ya kudhaminisha Gari (Fomu namba MMU 06)
- xii. Mkopaji atatakiwa kuwasilisha kwenye Chama, hati halisi ya Gari iliyowekwa rehani baada.
- xiii. Chama kutoa hati ya kuthibitisha kupokea hati halisi ya dhamana (Fomu namba MMU 07)
- xiv. Chama kitafanya usajili wa hati halisi ya dhamana kwa mamlaka husika (fomu namba MMU 07)
- xv. Mkopaji atajaza, atasaini na kuwasilisha hati ya ahadi (Fomu namba MU 04)
- xvi. Mkopo utatolewa
- xvii. Chama kitarejesha dhamana iliyowekwa rehani baada ya maresho ya mkopo kukamilika (Fomu namba MMU 08 na MMU 09)

b) Viambatanisho

- i. Hati ya Mshahara (payslip)
- ii. Nakala ya kitambulisho
- iii. Fomu ya Uhakiki wa dhamana ya mkopaji na/au mdhamini
- iv. Picha ya mkopaji na mwenza wakiwa mbele ya mali inayowekwa rehani
- v. Taarifa ya uthaminishaji wa mali (shamba/kiwanja/nyumba)
- vi. Hati ya kiapo cha kudhaminisha Garii (iambatane na 'cover note ya Bima 'comprehensive')
- vii. Hati ya kiapo cha mkopaji asiye na mwenza
- viii. Hati halisi ya mali ilyowekwa rehani

**Tanbihi:** Gari isizidi miaka 15 tangu ilipotengenezwa na isizidi cc 3,500

6. MAJINA YA WADHAMINI ISHIRINI (20) WALIOTIA SAINI ZAO KWA  
NIABA YA WANACHAMA WENZAO

Sisi tulioorodheshwa majina yetu na kusaini hapa chini, tunathibitisha kwa niaba ya Wanachama wote wa TANESCO SACCOS ya kwamba marekebisho ya sera hii yametayarishwa kwa mujibu wa Agenda namba 6 katika Mkutano Mkuu wa Mwaka 2018 wa TANESCO SACCOS uliofanyika tarehe 13.10.2018 katika ukumbi wa Kisenga International Conference Centre, Kijitonyama jijini Dar es Salaam, Tanzania na kuidhinishwa kwa usajili na Bodi ya Chama katika kikao cha tarehe 26.01.2019

Na.	Jina la Mwanachama	Saini	Tarehe
1			
2			
3			
4			
5			
6			
7			
8			
9			
10			
11			
12			
13			
14			
15			
16			
17			
18			

19			
20			